**Taarifa kwa Vyombo vya Habari**

**Mapendekezo Juu ya Kuboresha Mfumo wa Taasisi za Haki Jinai Nchini**

**Ndugu wanahabari,**

Itakumbukwa kwamba, Mnamo tarehe 06 mwezi Januari 2023 Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mh.Samia Suluhu Hassan alifanya uteuzi wa wajumbe wa Kamati ya kuangalia jinsi ya kuboresha taasisi za haki jinai nchini inayoongozwa na Mhe. Jaji Mkuu Mstaafu Othuman Chande na Makamu Mwenyekiti Katibu Mkuu Kiongozi Mstaafu Balozi Ombeni Yohana Sefue.

Itakumbukwa kwamba uteuzi wa wajumbe wa Kamati hii ni hatua muhimu wa kuifanya Kamati kuanza kazi yake kwa kuwa awali Rais aliteua Mwenyekiti na Makamu wa Kamati siku ya tarehe 20 Julai 2022 wakati akimuapisha Mkuu wa Jeshi la Polisi (IGP) nchini Camilius Wambura.

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) kinapongeza mwendelezo wa jitihada hizo zinazolenga kuboresha mfumo wa haki jinai nchini. Mara kwa mara, Mhe. Rais ametoa kauli chanya zenye nia ya kufanya maboresho makubwa ya mfumo wa haki jinai, mathalani mwezi Agosti, 2021 alinukuliwa na vyombo mbalimbali vya habari akisema kwamba uwekaji wa watu mahabusu kwa muda mrefu siyo tu unaleta mzigo kwa Serikali,bali ni ukiukwaji wa haki zao za msingi.Pamoja na hayo,alinukuliwa akieleza masuala mbalimbali yanayohusu haki jinai sambamba na kutoa maagizo mbalimbali kwa vyombo vya dola hususani Jeshi la Polisi na TAKUKURU kufanyia kazi masuala hayo ili kuboresha mfumo wa haki jinai nchini.

Mbali na kauli hizi, Serikali pia ilifanyia marekebisho Sheria ya mwenendo wa makosa ya jina kupitia sheria ya mabadiliko ya sheria mbalimbali namba 1 ya mwaka 2022 pamoja na mambo mengine sheria iliweka takwa la kufanya upelelezi kabla ya kumfungulia mtuhumiwa mashtaka.

**Ndugu wanahabari,**

LHRC imekuwa mstari wa mbele katika uchechemuzi wa Sheria kwa kupendekeza namna bora ya kuboresha mfumo wa haki jinai nchini ili kulinda Haki za Binadamu kupitia mifumo na taasisi za haki jinai nchini kama ilivyoelezwa kwa uchache katika jedwali hapo chini;

| Na. | Taasisi | Suala |
|---|---|---|
| 1. | Jeshi la Polisi na Polisi wasaidizi | Changamoto za weledi wa namna ya ukamataji, upekuzi, upelelezi na ugumu wa kutoa dhamana |
| 2. | Jeshi la Magereza | Miundominu chakavu, taratibu za upekuzi |
| 3. | Jeshi la Uhamiaji | Mfumo wa vibali |
| 4. | Mamlaka ya Kupambana na Kudhibiti Madawa ya Kulevya nchini. | Mamlaka hii ilijipa mamlaka ya Ukamataji, Upekuzi na Upelelezi kupitia mabadiliko na sheria mbalimbali No. 7 ya mwaka 2021. |
| 5. | Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Tanzania (TAKUKURU) | Ukamataji, Upekuzi na Upelelezi |
| 6. | Kamati ya Kupambana na Usafirishaji Haramu wa Binadamu | Ukamataji, Upekuzi na Upelelezi |
| 7. | Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka nchini | Kwenda mahakamani bila ushahidi/upelelezi kukamilika. |
| 8. | Kamishna wa Ustawi wa Jamii | Upungufu wa shule za maadilisho |
| 9. | Shule ya Maadilisho (Approved schools) | Miundominu si rafiki kwa ustawi wa mtoto ambapo hupelekea watoto kupelekwa kwenye magereza za watu wenye umri zaidi ya miaka 18. |
| 10. | Uwakilishi wa Kisheria kwenye kesi za watoto | Kumekuwa na changamoto iliyokithiri ya watoto wanaokinzana na sheria. |
| 11. | Rention homes | Zipo tano (5) tu Tanzania Bara; Arusha, Kilimanjaro, Dar es Salaam, Mbeya. |

| | | |
|---|---|---|
| | | Miundominu si rafiki kwa ustawi wa mtoto ambapo hupelekea watoto kupelekwa kwenye magereza za watu wenye umri zaidi ya miaka 18. |
| 12. | Majeshi usu katika Hifadhi za Taifa za Wanyamapori, mapori tengefu, misitu iliyochini ya Wakala wa Misitu Tanzania (mafunzo yao yawe chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani) | Ukamataji pamoja na kujichukulia sheria mikononi hasa kwa adhabu na shambulio linalopelekea vifo. |
| 13. | Mamlaka ya Serikali za Mitaa/Sungusungu/Migambo/Ulinzi shirikishi | Kuanzisha vikundi vya ulinzi ambavyo vingi havina uwezo na maarifa ya kutosha ya namna ya kushughulika na mhalifu. |
| 14. | Ofisi ya Kamishna wa Kazi | Ofisi hii imepewa jukumu la kipolisi, ambapo Kamishna wa kazi anaweza kutekeleza majukumu ya kipolisi ikiwemo ukamataji. |

**Ndg wanahabari**

Licha ya kamati teule ya Mhe Rais kupewa hadidu za rejea za kushughulika na taasisi nne pekee kwa maana ya ofisis ya DPP, TAKUKURU, mamlaka ya Madwa ya kulevya na jeshi la polisi, Kituo kinaona kuna haja ya kufanya mapitio ya taasisi nyinginezo zilizotajwa hapo juu zinazohusika moja kwa moja ama vinginevyo katika mfumo mzima wa haki jinai nchini, ili kulinda haki za binadamu, hususan haki za mahabusu, sambamba na kulinda haki za watu wanaowategemea, ikiwemo wanafamilia, ndugu, jamaa na marafiki.

Ripoti yetu ya Haki za Binadamu ya Mwaka 2020, iliangazia changamoto mbalimbali zinazohusiana na haki jinai, ikiwemo kasi ndogo ya uchunguzi/upelelezi wakati watuhumiwa wapo mahabusu au gerezani na ubambikizaji wa kesi.

Ripoti hiyo iliainisha kwamba kwa mwaka 2020, mahabusu 1,422 waliachiwa na Mkurugenzi wa Mashitaka baada ya kubainika kwamba walikuwa wamebambikiwa kesi.

Hali kadhalika, Ripoti ya Haki za Binadamu ya Mwaka 2021 ilijikita katika haki jinai, ambapo kauli mbiu ya ripoti hiyo ilikuwa ni;

Kwa mujibu wa ripoti hii, wanajamii wengi walioshiriki katika ufatifi 49% walisema pia kwamba ubambikaji wa kesi ni tatizo kubwa katika jamii zao, wakifuatiwa na waliosema ni tatizo kiasi 38%. Ripoti inaongezea kwamba mnamo mwezi Mei mwaka 2021,iliripotiwa kwamba kesi 147, ambazo zilionekana ni za kubambika, zilifutwa na TAKUKURU.

Kwa upande mwingine, kuna changamoto ya kesi kupelekwa mahakamani kabla ya upelelezi kukamilika, ripoti imeainisha kwamba, kulikuwa na takribani kesi 19 za uwekaji kizuizini kwa muda mrefu.

Kwa mwaka 2021, LHRC ilitoa ripoti maalum kuhusu makosa yasiyokuwa na dhamana, ripoti hiyo ili toa mapendekezo ya kufanya maboresho ya mfumo mzima wa haki jinai ili kuhakikisha haki za mtuhumiwa zinalindwa. Aidha, LHRC ilipendekeza kuwepo na ukomo wa upelelezi wa makosa ya jinai, kuipa Mahakama uwezo wa kusikiliza na kutoa dhamana katika makosa yote.

Ikumbukwe kwamba, chini ya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai,1985 kama ilivyofanyiwa marejeo mwaka 2022, Mahakama ilikuwa na uwezo wa kusikiliza maombi na kutoa dhamana katika makosa yasiyokuwa na dhamana kabla ya kuondolewa.

**Ndugu wanahabari,**

Itakumbukwa kwamba siku za hivi karibuni, kumeripotiwa matukio mbalimbali ya kikatili dhidi ya watuhumiwa wa makosa ya jinai ambayo kwa kiasi kikubwa yameathiri haki za msingi za watu hao, kwa mfano, kumekuwa na mtindo wa vikundi vya jadi maarufu kama sungusungu kujivika mamlaka ya kipolisi ikiwemo kukamata na kujichukulia sheria mikononi, kwa mfano tukio la hivi karibuni mkoani Arusha wilayani Arumeru la kijana aliyepigwa na kikundi cha sungusungu hadi kupoteza maisha. Hii inatokana na vikundi hivi vya jadi kutokuwa na uwezo wala weledi wa kushughulika na wahalifu.

Pamoja na nia ya Serikali ya Rais Samia ya kuboresha hali ya haki jinai nchini, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kinapenda kutoa mapendekezo yafuatayo ili kuweza kufikia vizuri na kwa ufanisi azma hii:

**Mapendekezo ya Jumla**

1. **Kutumia mchakato wa Katiba ili kuimarisha mfumo wa taasisi za haki jinai na kuweka taasisi zake kuwa za kikatiba, mathalani;**

i. Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), kimsingi hii ni ndio taasisi mama yenye mamlaka ya kudhibiti na kupambana na Rushwa nchini, hivyo ni muhimu kwa taasisi hii kuwa taasisi ya kikatiba ili kuifanya kuwa taasisi imara na yenye weledi na huru.

ii. Ofisi ya Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai nchini (DCI) ikiwa ni taasisi mama yenye mamlaka ya upelelezi wa makosa ya jinai nchini. Hivyo ni muhimu kwa taasisi hii kuwa taasisi ya kikatiba na kuitenganisha ofisi hii kutoka kuwa sehemu ya Jeshi la Polisi na kuwa kurugenzi inayojitegemea kama ambavyo wenzetu wa Kenya na Afrika ya Kusini wamefanya. Hatua hii itaifanya taasisi hii kuwa taasisi imara na yenye weledi zaidi na huru.

iii. Kuundwa kwa chombo huru kitakacho shughulika na mwenendo na utendaji kazi wa Jeshi la Polisi hapa nchini.

iv. Kutenganisha majukumu ya Taasisi au Mamlaka zinazohusika na haki jinai, kwa mfano, Mamlaka ya Kupambana na Madawa ya Kulevya Nchini kufanya kazi za kisera, elimu kwa umma, utalaamu na intelijensia pekee. Tofauti na sasa ambapo mamlaka hii imepewa majukumu ya kipolisi ikiwemo kazi za upekuzi, upelelezi na ukamataji. Ni busara jukumu la ukamataji, upekezi na upelelezi ukabaki kuwa jukumu kuu la jeshi la polisi. Miaka ya hivi karibuni taasisi mbalimbali zinazohusika ama moja kwa moja au vinginevyo na mfumo wa haki jinai zimekuwa zikijivika jukumu la kipolisi kama vile ukamataji, upekuzi na upelelezi, mfano wa taasisi hizo ni kama vile,TRA,kamishina wa kazi, mamlaka ya kupambana na madawa ya kulevya, TAKUKURU, Kamati ya kupambana na usafirishaji haramu wa Binadamu. Ni vyema kazi hizi zikabaki kwa jeshi la polisi.

v. Mahakama kuwa na mamlaka ya kutoa dhamana kwa makosa yote kwa masharti na taratibu maalumu kulingana na mazingira kesi.

vi. Kuondokana na adhabu kali na vifungo vya muda mrefu ili kupunguza msongamano magerezani na kusimarisha Parole Board.

vii. Kuondokana na adhabu ya kifo kwani adhabu hii inatweza utu, ya kikoloni na haitekelezeki.

**Mapendekezo kwa Kamati**

2. Kamati teule ya Rais ialike wadau pamoja na kutoa ratiba (*public hearing*) ili kutoa fursa kwa wadau mbalimbali kupeleke mapendekezo na maoni ya kuboresha mfumo wa haki jinai nchini, pendekezo hili litaisaidia Kamati kuja na taarifa yenye wigo mpana

wa mapendekezo kutoka kwa wadau mbalimbali na jamii kwa ujumla.Sambamba na hilo, hatua hii itasaidia kupunguza malalamiko miongoni mwa wadau.

3. Kupitia upya mfumo wa upelelezi kuendana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia.
4. Pia, kuweka kipaumbele cha kuboresha sheria kama zilivyoainishwa kwenye jedwali lifuatalo;

| Na. | Jina la Sheria |
|---|---|
| 1. | Sheria ya Kudhibiti Madawa ya Kulevya, 2015<br>Drugs Control and Enforcement Act, 2015 R.E 2019 |
| 2. | Sheria ya Taasisi ya Kudhibiti na Kupambana na Rushwa, 2007<br>Prevention and Combating of Corruption 2007 |
| 3. | Sheria ya Kudhibiti Uhujumu Uchumi, Sura 200<br>Economic and Organized Crime Control Act Cap 200 |
| 4. | Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, 1985<br>Criminal Procedure Act, 1985 |
| 5. | Sheria ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu, 2008<br>Anti-Trafficking in Persons Act 2008 |
| 6. | Kanuni ya Adhabu, Sura 16<br>Penal Code Cap 16 |
| 7. | Sheria ya Makosa ya Mtandaoni, 2015<br>Cybercrimes Act, 2015 |
| 8. | Sheria ya Huduma ya Vyombo vya Habari, 2016<br>Media Services Act, 2016 |
| 9. | Sheria ya Mtoto, Namba 21, 2009<br>Law of the Child Act No.21 of 2009 |
| 10. | Inquest Act Cap 24 |
| 11. | Sheria ya Kuzuia Utakatishaji Fedha, 2006<br>Anti-Money Laundering Act 2006 |
| 12. | Firearms and Ammunition Cap 223 |
| 13. | Sheria ya Jeshi la Polisi na Huduma Saidizi, Sura 322<br>Police Force and Auxiliary Services Act Cap 322 |
| 14. | Permanent Commission of Enquiry 1980 |
| 15. | Deportation Act, 1991 |
| 16. | Sheria ya Umeme, Sura 131<br>Electricity Act Cap 131 |
| 17. | Energy and Water Utilities Regulatory Authority Act |

| | |
|---|---|
| 18. | Sheria ya Ushahidi, Sura 6<br>Evidence Act Cap 6 |
| 19. | Explosive Act Cap 45 |
| 20. | Sheria ya Uvuvi, Sura 279<br>Fisheries Act, Cap 279 |
| 21. | Sheria ya Uhamiaji, Sura 54<br>Immigration Act Cap 54 |
| 22. | Expulsion of Undesirable Person Cap. 39 |
| 23. | Destitute Act Cap 389 |
| 24. | Sheria ya Magereza, 1967<br>Prisons Act, 1967 |
| 25. | Proceeds of Crime Act, Cap 256 |
| 26. | Sheria ya Wakimbizi, Sura 37<br>Refugee Act, Cap 37 |
| 27. | Sheria ya Tawala za Mikoa, 1997<br>Regional Administration Act, 1997 |
| 28. | Resettlement of Offenders Cap 71 |
| 29. | Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania, Sura 399<br>Tanzania Revenue Authority Act, Cap 399 |
| 30. | Wildlife Conservation Act Cap.283 |
| 31. | Sheria ya Uchawi, Sura 18<br>Witchcraft Act, Cap 18 |

**Imetolewa leo tarehe 02 Februari, 2023 na;**

**Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC)**

**Anna Henga (Wakili)**

**Mkurugenzi Mtendaji**